

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

Simu: +255 (0) 26 2322602
Tovuti: www.maji.go.tz
Barua pepe: ps@maji.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtaa wa Maji,
S. L. P. 456,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI KITAIFA 2024



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Maji Duniani. Mwaka 1993 Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira na Maendeleo lilipitisha Azimio rasmi la kuadhimisha Siku ya Maji Duniani kila mwaka ifikapo tarehe 22 Machi.

Siku hii hufanyika ili kutambua umuhimu na thamani ya maji katika maisha ya binadamu na uchumi wa dunia kwa ujumla. Lengo ni kuipa fursa Sekta ya Maji kujipima na kuwafahamisha wananchi kuhusu mafanikio yaliyofikiwa na kubainisha njia za kutatua changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Maji, Sheria na Miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutathmini utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji inayolenga kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji safi na salama.

Maadhimisho kwa mwaka 2024 yatafanyika Jijini Dodoma na kaulimbiu ya maadhimisho ya dunia ni **“Uhakika wa Maji kwa Amani na Utulivu”**. Kauli mbiu hii inalenga kuyafanya maji kuwa nyezo muhimu katika kuleta amani na umoja.

Kaulimbiu ya kitaifa itahusu utunzaji wa vyanzo vya maji ambayo ni **‘Uhakika wa Maji kwa Amani na Utulivu’**. Maadhimisho yataambatana na Wiki ya Maji kuanzia tarehe 16-22, Machi 2024 yatakayotumika kuonesha kazi mbalimbali zinazotekelezwa kwenye Sekta ya Maji ikiwamo matukio makuu sita kama ifuatavyo:-

1. Matembezi ya Wiki ya Maji, kuanzia na kuishia Ofisi ya Wizara ya Maji, Mji wa Serikali Mtumba tarehe 16 Machi, 2024 - Dodoma.
2. Uwekaji wa mawe ya msingi na uzinduzi wa miradi ya maji, tarehe 16-21 Machi, 2024.
3. Siku ya EWURA-Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka za Maji, tarehe 18-19 Machi, 2024 Dodoma.
4. Mkutano wa Mapitio ya Sekta ya Maji Nchini, tarehe 20-21 Machi, 2024, Dodoma;

Siku ya Kilele cha Wiki ya Maji tarehe 22 Machi, 2024.

5. Wanawake na Maji, uzinduzi wa miradi ya visima katika maeneo mbalimbali.
6. Shughuli za utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali.

